**EPISODE 6 "THE SERVICE CENTRE"**

**SCRIPT WRITER** **Njoki Muhoho**

**EDITOR** **Jan-Philipp.Scholz**

**KISUAHELI:** **Eric Ponda**

**CHARACTERS**

| | |
|---|---|
| **ANNOUNCER** | Male Adult |
| **ZAPCOM** | A 23-year-old computer geek, by village standards. |
| **GEORGE** | 20 years old. Waits tables at his Uncle Kilu's restaurant. |
| **UNCLE KILU** | 55 years old. George's uncle, owner of KULA TU FOODS. |
| **OMWA** | 19 years old and jobless. Female. |
| **KAMAU** | A customer. (M/F) |

**INTRO**

1. **MUSIC: THEME MUSIC**

2. **ANNOUNCER** HUJAMBO MSIKILIZAJI MAHALI POPOTE ULIPO. NI WAKATI MWENGINE TUNAPOUNGANA NAWE KUKULETEA MAKALA NYINGINE YA 'LEARNING BY EAR' NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO, TUKIWA

BADO TUNAZUNGUMZIA TEKNOLOJIA MPYA YA HABARI NA MAWASILIANO.HIKI NI KIPINDI CHA 6 KATIKA MFULULIZO HUU KWA JINA "KITUO CHA HUDUMA ZA INTANETI".

KATIKA KIPINDI KILICHOTANGULIA ZAPCOM NA WASHIRIKA WAKE WA KIBIASHARA WANAFAHAMU KWAMBA MTU ANAPOKUWA NA KIFAA CHA MAWASILIANO KAMA SIMU YA MKONONI,NI MANUFAA MAKUBWA MBALI YA KUPIGA AU KUPOKEA SIMU..LAKINI PIA WANAFAHAMU HUDUMA HIZI ZINAAMBATANA NA CHANGAMOTO NYINGI TU, KAMA VILE USALAMA WA MALIGHAFI INAYOTUMIWA KUTENGENEZA VIFAA HIVI, NA NJIA SALAMA YA KUTUPA TAKA KUTOKA KWA BIDHAA ZA ELEKTORNIKI.
JE NI YAPI WATAKAYO JIFUNZA ZAIDI KUTOKANA NA TEKNOLOJIA HII MPYA YA HABARI NA MAWASILIANO…… MENGI ZAIDI ENDELEA KUWA NASI HADI MWISHO WA KIPINDI.

**3. A-SFX: PHONE KEYBOARD TAPPING**

**SCENE 1: KULA TU FOODS**

| | | |
|---|---|---|
| **4.** | **UNCLE KILU** | **(WHISPERING)**….Nakwambia huyu ni msichana mvivu sana!.Kazi yake ni kukaa tu na kushika shika simu yake ya mkononi kila mara. Mimi siwezi kumuajiri mtu kama huyu katika mgahawa wangu wa Kula Tu Foods. |
| **5.** | **ZAPCOM** | Nani huyo? |
| **6.** | **UNCLE KILU** | Si ni Omwa!. |
| **7.** | **ZAPCOM** | Oh, yule?.. hana shida . |
| **8.** | **UNCLE KILU** | Hebu ngoja tu kidogo nitakuonyesha **(CLEARS THROAT and SHOUTS ACROSS)** Omwa?... Omwa? Wewe msichana … nahitaji msaada wako!. Tafadhali nifanyie hesabu hii? |
| **9.** | **OMWA** | (**DISTRACTED**).Basi niambie tu nambari na bila shaka nitakufanyia. Ni hesabu gani hiyo!. |
| **10.** | **UNCLE KILU** | (**ANNOYED**) Nini? (**TO ZAPCOM**) Sasa unaona! |
| **11.** | **OMWA** | (**SHOUTING ACROSS**) Niambie hizo nambari mjomba, ni gani hizo…? |

**12. ZAPCOM** (**BEMUSED**) Mwambie, …msomee hizo nambari!.

**13. UNCLE KILU** (**UNCONVINCED**), 2,345 ongeza 43 ongeza 1238 ongeza 11630 (**ANNOYED**).Unaandika au napoteza wakati wangu tu bure..!

**14. OMWA** Ni 15,213!

**15. UNCLE KILU** Eti nini?

**16. OMWA** Ndio jibu lako hilo, au una nyingine?

**17. ZAPCOM** (**BEMUSED**) Mzee yule msichana hachezi na simu pale, anatumia kikokotoo kwenye simu hiyo ya mkononi!.

**18. UNCLE KILU** Oooh

**19. ZAPCOM** Ni vyema pia wewe uwe na simu ya mkononi!.

**20. UNCLE KILU** Mimi…! , ya kazi gani? Nikihitaji utaniazima yako.

**21. ZAPCOM** Hebu tazama ...!

**22. B-SFX: PAPERS RUFFLE AS HE SPREADS OUT A MAGAZINE.**

**23.** **ZAPCOM** Nilipata jarida hili kutoka kwa shangazi Bongi. Hebu tazama hii simu, hii inakufaa kabisa, na bei yake ni ……. (**PAUSE**) (**SHOUTING TOWARDS OMWA**)… Omwa, dola 50 ni pesa ngapi za humu nchini.?

**24.** **UNCLE KILU** (**SNEERING**) Tangu lini Omwa akawa mtaalam wa masuala ya ubadilishanaji wa fedha?

**25.** **OMWA** Kufikia jana dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa shilingi 12,000.

**26.** **UNCLE KILU** (**SHOCKED)…** Eehe… umejuaje?…Kumbe unajua……! lakini huyu hanywi supu ya mbuzi, inakuwaje ni mwerevu hivi.?

**27.** **ZAPCOM** Tangu aanze kutumia huduma hii ya simu ya mkononi.

**28.** **UNCLE KILU** Unajua nimekuwa nikifikiria nini kumhusu msichana yule? Ni mvivu tu!

**29. ZAPCOM** Ondoa kabisa dhana hizo, kuwa na imani … teknolojia mpya ya mawasiliano sio tu inakufungulia mlango wa ulimwengu mzima bali akili pia. Simu ya mkononi ndio chombo unachokihitaji wakati wote mahali popote, iwe ni kupiga simu, kusikiliza redio, kutumia kikokoroo, na hata huduma nyinginezo. Nipe tu shilingi 12,000 pamoja na nauli nitakuletea simu mpya!

**30. ANNOUNCER** Teknolojia mpya ya mawasiliano na simu ya mkononi inaendelea kuleta maajabu katika kijiji hiki. Na unaweza kujifunza mengi kuhusu matumizi na huduma zinazopatikana katika kifaa hiki. Lakini yote haya yanategemea juhudi za mtu binafsi. Simu ambayo mjomba Kilu alidhania ni chombo tu cha burudani kwa vijana, sasa imebainika kuwa raslimali kubwa katika kuboresha biashara yake. Hiyo ndiyo lugha anayoielewa vyema. Biashara!

**SCENE TWO: INTERNET CAFÉ CORNER AT KULA TU FOODS**

**31. C-SFX: HESITANT TYPING ON KEYBOARD. A CLOCK ALARM GOES OFF.**

**32. OMWA** Oh siamini usiku umeingia haraka hivi..!

**33. ZAPCOM** (**HANDING HER HIS PHONE**) Saa zimekwisha. Muda wako wa saa moja kujifunza kupiga chapa umemalizika. Sasa rudi ofisni uendelee na kazi zako za kawaida.

**34. OMWA** Tafadhali nipe dakika 15 tu… sasa nimeanza kuzoea.

**35. ZAPCOM** Sawa basi dakika 15 tu! Kengele ya saa kwenye simu yangu ya mkononi hulia kila baada ya dakika 15, kwa hivyo ukisikia ikilia ujue muda wako wa dakika 15 umekwisha. Si lazima nikukumbushe. ..sawa?.

**36. OMWA** Sawa..!kumbe sasa teknolojia mpya imeanza kukufanyia kazi?.

**37. ZAPCOM** Ndio uzuri wa teknolojia hii. Sasa unaendelea kupoteza muda zaidi ukizungumza na mimi badala ya kufanya kazi yako. Hebu endelea na kazi yako ya kuandika!

**38. D-SFX: CHAIR CRASHES AS SOMEONE STANDS UP IN A HURRY**

**39. OMWA** Oooh, nimesahau!

**40. ZAPCOM** Umesahau nini?

**41. OMWA** Nahitaji kuchukua picha zangu za pasipoti na kuzituma kwa jamaa zangu jijini. Studio huenda itafungwa katika muda wa 15 zijazo … (**PAUSE**)… ohh na sasa angalia ni saa ngapi! Ni vyema niende sasa!

**42. ZAPCOM** (**CALMINGLY**) Usijali, keti uendelee na mafunzo haya ya kupiga chapa kwanza. Kisha ukimaliza unaweza kupiga picha kwa kutumia simu yako ya mkononi na kuzituma.

**43. OMWA** Inawezekana? Hebu tujaribu kwanza!

**44. E-SFX: CAMERA FLASHES AS THEY TAKE PICTURES.**

***45.*** **ZAPCOM** Ahhh, unaweza kupiga picha nzuri zaidi ya hiyo. Hii ni kama zile za watu wanaotafutwa na polisi, ambazo hutundikwa kwenye kuta za kila kituo cha polisi na maandishi makubwa ya '***ANATAFUTWA!'.***

**46. OMWA** Hebu nione… yuk…ni kweli ni mbaya sana!

**47. ZAPCOM** Nimeifuta. Tupige nyengine… tabasamu basi… tayari,….tabasamu…na sasaaa…

**48. F-SFX: MORE SOUNDS OF CAMERA FLASHES AND GIGGLING**

**49. UNCLE KILU** Hehehe… kunaendelea nini hapa? Kwani hamna kazi ya kufanya isipokuwa kucheza tu kama watoto?.

**50. G-SFX: MORE CAMERA FLASHES**

**51. UNCLE KILU** Hebu ondoa haraka simu yako mbele ya uso wangu!.

**52. ZAPCOM** OMWA, nipe huo waya wa USB.

**53. ZAPCOM** (**LAUGHS**) Hii utaipenda…?

**54. OMWA** Unafanya nini Zapcom?

**55. ZAPCOM** Nataka kuweka hizi picha zote nilizopiga kwa komputa.

**56. UNCLE KILU** Ha… asaaalalaa…Simu yako pia inachukua picha sasa…! Hebu angalia macho yangu, yanafanana na ya babu…!

**57. ZAPCOM** Omwa, nitakutumia picha zako kupitia baruapepe kisha unaweza kuzituma kwa mtu yeyote mahali popote.

**58. OMWA** Asante sana umeokoa pesa na muda wangu pia. (**SMACK KISS**) Zapcom!

**59. UNCLE KILU** **(TEASING)** Hakuna kubusiana mbele yangu… heee? Na hiyo…, sura yangu inafanya nini kwa komputa?

**60. H-SFX: MUTED MUSIC**

**61. UNCLE KILU** George, na hakika rafiki zako watakuwa na hamu ya kuiuza picha yangu.

**62. (SILENCE)**

**63. UNCLE KILU** **(SHOUTING)** George! Umerudisha tena hizo spika kwa masikio yako, kwani bado unasikiliza redio?

**64. I-SFX: MUTED MUSIC DIES**

**65. GEORGE** Samahani mjomba, unazungumza na mimi?

**66. UNCLE KILU** Ehhh nazungumza na wewe! Mimi napiga makelele hapa na wewe husikii. Kwani ni stesheni gani unayosikiliza ambayo hata huwezi kusikia kinachoendelea?

**67. GEORGE** Si redio, nasikiliza muziki kutoka simu yangu ya mkononi.. (**PAUSE AS HE HANDS THE EAR PHONES**) Hebu sikiliza, pia wewe utaupenda.

**68.** **UNCLE KILU** Nini kinachokufanya ufikirie nitazipenda hizo kelele unazoziita muziki?. Hata hivyo nilikuwa namuuliza rafiki yako hapa, picha zangu zinafanya nini kwa komputa..?

**69.** **ZAPCOM** Unaweza kuzichapisha na kuwapa …

**70.** **GEORGE** **(INTERRUPTS)…** Au kuiweka katika skrini za komputa zetu zote…kwa lugha ya kitaalam ***Screne Saver*** ..

**71.** **UNCLE KILU** Eti nini?

**72.** **ANNOUNCER** Kama kuna wakati Mjomba Kilu amekuwa na furaha isiyo na kifani basi ni siku ya leo. Sasa wateja wote wanaokuja katika mgahawa na kutumia komputa hizi pia watakuwa na fursa ya kuona picha yake kwenye skrini. Ama kwa hakika teknolojia hii inamweka mbele zaidi kibiashara kuliko washindani wake.

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**SCENE THREE: KULA TU FOODS LATE AFTERNOON**

**73.** **UNCLE KILU** **(FIRM)** George, Nakwambia tusithubutu kuweka picha ya Kamau hapa. Ni Mtu muongo na kazi ni kula tu bila kulipa..

**74. GEORGE** Usijali mjomba, mimi na Zapcom tutaikomesha tabia yake. Hebu twende tukazungumze na Kamau. Na kisha beba simu ya Zap.

**75. UNCLE KILU** Kamau, pesa zangu ziko wapi. Uliniahidi kunilipa leo.. wapi pesa zangu?.

**76. KAMAU** Pesa gani…? Siku gani mimi nilikuahidi kukulipa pesa zozote… lini ? Wewe Mzee, usinikosee heshima, nadhani umeanza kushikwa na wazimu.Wewe hunidai chochote! George, hebu niletee chai na chapati tafadhali.

**77. ZAPCOM** Kamau, Utaletewa lakini kwanza sikiliza huu muziki.

**78. KAMAU** (MOCKING) Nini…..? Muziki kutoka kwa simu ya mkononi?

**79. GEORGE** Hapana , hapana wewe, na subiri kusikia ahadi zako za uongo kwa mjomba Kilu. Ni lini utamlipa mjomba deni la chakula ulichokula.

**80. J-SFX: MUMBLING OF A RECORDING THAT GETS CLEARER**.

**81. KAMAU(VO)** Usijali Mzee, nitakulipa deni lako punde tu nitakapolipwa mshahara wangu!.

**82.** **UNCLE KILU(**VO) Unahakika?

**83.** **KAMAU(VO)** Nakuapia kwa kaburi la marehemu mamangu…!

**84.** **K-SFX: ABRUPT END TO RECORDING.**

**85.** **UNCLE KILU** Tafadhali usimtaje marehemu mamako katika suala hili, wacha roho ya mamako ilale mahali pema peponi.Unapasa kumridhisha mahali aliko. (**SHOUTING**) Nilipe pesa zangu sasa hivi au niwaite walinzi kukutoa nje.

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**86.** **ANNOUNCER** Mjomba Kilu na kundi zima la vijana hawakutarajia manufaa wanayoshuhudia kutokana na huduma hii ya teknolojia mpya ya mawsiliano. Ama kwa hakika imebadilisha kabisha maisha na hata kuboresha biashara yao. Biashara ya mgahawa wa Kula Tu Foods ambao ni wa kawaida katika sehemu za mashambani sasa inazidi kuimarika kutokana na Teknolojia hii. Mjomba Kilu bado anatafakari jinsi kifaa kidogo kama simu ya mkononi inavyoweza kumletea mabadiliko makubwa maishani.

**87. GEORGE** Zapcom, Uliwezaje kuweka picha hizi ulizopiga kwa kutumia simu yako ya mkononi kwenye komputa?

**88. ZAPCOM** Nimetumia waya unaofahamika kama ***USB cable***. USB ina maana ***Universal Serial Bus***. Hutumika kuhamisha habari au picha hadi kwa kwa komputa. Ni teknolojia ya kisasa kabisa ambayo inakuwezesha kuunganisha kwa urahisi vifaa vingine vya mawasiliano kama vile simu za mkononi, kamera, au kutoka kwa mashini za uchapishaji hadi kwa komputa. Kwa lugha ya kitaalam teknolojia hii inajulikana '***plug and play'*** yaani kuchomeka na kutumia kutokana na urahisi wake wa matumizi.

**89. GEORGE** Ohhh mungu wangu! Kumbe bado kuna mengi ya kujifunza kutoka kwa teknolojia hii ya simu ya mkononi.

**90.** MUSIC: THEME MUSIC

OUTRO

**91. ANNOUNCER** Ama kwa hakika elimu haina mwisho. Bado kuna mengi tu sana ya kujifunza , kama vile

sheria zinazosimamia haki ya kutumia tovuti mbali mbali kwenye mtandao. Je ni yapi watakayojifunza baadaye. Kwa mengi zaidi ungana nasi kwa makala yajayo ya "Learning By Ear" Noa Bongo jenga maisha yako.

**92.**

**93.** Pia kwa maelezo zaidi kuhusu vipindi vya Learning By Ear au ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki unaweza kutembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe.

Na iwapo unamaoni pia usisite kututumia nasi bila shaka tutayapokea kwa moyo mkunjufu.Hadi wakati mwengine tutakapoungana tena kukuletea makala nyingine Kwaheri kwa sasa..